786
JANUWARI 2023 TOLEO 03
GOMBO LA ISIMU TUMI

# NI KUFUWATA SAṮI ZA MAJAGINA WA ISIMU

DKT. MOHAMED KARAMA, UNIVERSITY OF KABIANGA

## Haya ya wababa na wamama ṇyapi tena?

Katika ṯembeyaṯembeya zangu huku Mwambatsa husikiya kiSwahili ambacho hunishangaza nikabakiya kujiuliza, “Mambasa iṇkuwa Kabianga?!” Kwamba Kabianga kwasemwa “kibara” (mchanganyiko wa kiSanifu na kiSheng) chembelecho Mazrui na Njogu (2022) walivomaanisha katika *Mikondo ya Kiswahili*, si bina. Ajabu ni mSwahili kiṇḏi kiṇḏaki, lugha na uṯamaḏuni, au mwalimu wa sarufi ya kiSwahili nawo wanena “wababa”, “wamama”! Watumiyaji wa lugha hawalaumiki kwa sababu huweza kutumiya kiyasi ya kwa kuwako “wa-vulana”, “wa-sichana”, “wana-hewa” basi na “wa-baba” na “wa-mama” piya iṯakuwako. Walakini, ukiwauliza, mbona katika kiSwahili tʰwasikiya “ma-babu”, “ma-bibi” na hatujasikiya “wa-babu” na “wa-bibi”? Waṯakujibu hawajuwi kwa nini. Tʰwaweza kukubaliyana na mawazo ya waṯaalamu tuliyowaṯaja kwamba makutano ya lugha ṯafauṯiṯafauṯi husababisha mkopano lakini makala haya yaṯaonesha ni mbabaisho unawoṯokana na wanasarufi kuṯoweka wazi mifumo ya Sarufi Maumbo ya lugha hii ya kiSwahili. Kusuluhisha mbabaisho huu, makala haya mafupi yaṯadhihirisha kuwa maneno haya ya mahusiyano ya kijamii (kwengine huitwa ya ukoo) ni ya mkopo, na sarufi ya kiSwahili imeweka ṯaraṯibu zake kuhusu maneno ya mkopo.

Maneno haya ya kyukoo yaliyanza ni ‘majina’ katika *Sarufi ya Kiswahili* (Mbaabu, 1985) na kuwa ‘nomino’ ikifikiya *Muundo wa Kiswahili* (Obuchi & Mukhwana, 2015). Nomino hizi hupangwa kwenye ngeli (makunri) ṯafauṯiṯafauṯi kulingana na: maumbo ya miyanzo (mofolojiya); maana inayobebwa (semantiki); na uwamilifu kimuunro (sintaksiya). Vigezo hivi vitatu nrivo huraṯibisha nomino zoṯʰe katika kiSwahili. Kwa mfano:

1) **M**sichana **a**mekwenra shule.
2) **Wa**sichana **wa**mekwenra shule.

Katika mfano huwo, kulingana na *Mtalaa wa Isimu* (Mgullu, 1999) ngeli za kiSwahili hupangwa kyumoja na kiwingi na nomino hapo ni ‘m-sichana’ na ‘wa-sichana’. Kimofolojiya, tuṯasema ‘-sichana’ iko katika ngeli ya M-WA (zenye mkolezo) kuṯokana na miyanzo ya maneno hayo. Kisemantiki, nomino hizo mbili ziko pamoja na majina ya kipekee na kawaiḏa ya binaḏamu (Mary, James, mwanasheriya, mwanamuziki) na wanyama (simba, ng’ombe, mbuzi) piya—vitʰu venye uhayi isipokuwa mimeya—chembelecho Sarufi Mapokezi. Kisintaksiya, na hili lililetwa ‘kusuluhisha matatizo’ (nimeweka kwenye madonroo kurejeleya tafsili barabara za Obuchi & Mukhwana kuhusu ngeli na kusaili faida yake katika mofofonolojiya) ya vigezo va mwanzo tulivoṯaja, baḏala ya miyanzo na maana ya nomino, tutumiye viyambishi va kiima katika fungutenzi yaani A-WA (zenye mkolezo). Kwa kuwa masṯaajabu yetu kuhusu ‘wa-baba’ na ‘wa-mama’ ni masiyala ya kimofolojiya na kisemantiki basi tuṯajikita kwenye vigezo hivi kwa sababu kigezo cha kisintaksiya nomino hizi (‘baba’, ‘mababa’, ‘mama’, na ‘mamama’ kama tuṯakavofafanuwa) ni A-WA vilevile.

**Jeḏwali 1: Maneno ya Ukoo kwenye Lugha za Kenya**

| **kiSanifu** | **ekeGusii** | **kiMaragoli** | **kiGĩkũyũ** | **kiSwahili Asiliya** | **kiKipsigis** | **kiUrḏu** | **kiArabu** | **kiIngereza** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mama | Baba/Mama | Mama/Nyina | Mami/Maitũ | Inya/Nina | Koruchon | Maa | Mama | Mother |
| Baba | Tata/Ise | Baba/Ise | Fafa | *Ishe | Pamong'o | Baap | Baba | Father |
| Babu | Sokoro | Guga | Guka | Shekuwe/Bibi | Potich | Dada/Babubha | Habib | Grandfather |
| Nyanya | Magokoro | Guku | Cũcũ | Nyanya | Patiem | Dadi | Hababah | Grandmother |
| Bibi | Omokungu | Mkari | Mũtumia/Mũka | Mke | Kwondo/Osotiot | Bibi | Sayyidah | wife |
| Bwana | Omogaka | Msaza | Mũthuri/Mũrũme | Mvuli | Manung'otiot | Shohar | Sayyid | Husband |
| Kaka | Omomura | Amwavo | Mũro wa maitũ | Abawa | Ng'etab Kam | Bhai | Akh | Brother |
| Dada | Omosubati | Mbozo | Mwarĩ wa maitũ | Abaya/Yaye/Kake | Chepkam | Bahan | Ukht | Sister |
| Shangazi | Mamamoke/ Omoko | Senge/Shenje | Tata | Shangazi | Senge/Mbocho | Chachi | Ammat | Paternal Aunt |
| Mjomba | Mame | Koza | Mama | Avu/Baṯiṯi | Umama | Chacha | Khal | Maternal Uncle |
| Halati/Hale | Mamamoke | Mshara | Tata | #Aji [aʥi]/Maṯiṯi | Kamatit | Masi | Khaleh | Maternal Aunt |
| Shemeji | Omoko | Semeji/ Mulamwa | Maramu | Muwamu | Pomuru | Chiyetah | Sohru | Brother in law |

UFUNGUWO

| | |
|---|---|
| | Mkopano wa ukaribu jamii mbalimbali |
| | Mfanyiko wa kimofolojiya |
| | Upatikanaji kisadfa |
| | Kupatikana ulimwenguni mwoṯ$^{h}$e |

* Nomino hii na nyenginezo zinaweza kuwa na kivumishi kimilikishi lakini tusizichukuliye kwa sasa.
# Nomino hii niliipata kwa Ustadh Ahmad Nassir. Mtaani Mji wa Kale, Mambasa kulikuwa na mt$^{h}$u-mzima mmoja, namkumbuka, akiitwa /ashṯ*ma/. Kwa hivo, nomino hii ikitufikiya makamu yetu kwisikiya ṯayari sauṯi ishabaḏilika kuṯoka /ʥi/ haḏi /sh/.

Jeḏwali hilo linaonesha nomino za ukoo zinavosemwa kwenye lugha hizo tulizochaguwa kimakusudi kwa kumili (niliwauliza wanafunzi wangu wa kiSwahili, UoK ṯu) isipokuwa kiUrḏu, kiArabu, na KiIngereza ambazo data yake tuliipata kwa kutumiya tafsiri ya Google na kuuliziya kwa wachache. Mifanyiko kadhaa yanadhihirika: 1) Kuna kukopana baina ya lugha za jamii moja (za kiBantu [kiGĩkũyũ, kiAsiliya, kiMaragoli]), jamii mbili ṯafauṯi za karibu (ekeGusii na kiKipsigis), au jamii mbili ṯafauṯi za mbali (kiArabu/kiUrḏu na kiSanifu); 2) Kujenga misamiyaṯi kwa mbinu moja ya kimofolojiya—kwambisha: ‘sokoro’ (ekeGusii) na ‘shekuwe’ (kiAsiliya) zoṯʰe zimeṯokana na ‘ise’ + ‘koro/kuu’ yaani ‘baba mkuu’; 3) Kuṯokeya neno kisadfa katika lugha mbili au zaiḏi zisizo na uhusiyano katika nomino ‘tata’ na haṯa katika kiMaya (lugha ya Belize, Amerika ya Kati) neno ni lilo kwa maana ya ‘uncle’ (Yule, 2010 uk. 268); 4) Kupatikana kwa neno ulimwenguni mwoṯʰe ‘ba’ na ‘ma’.

**Baba na mama ni ya mkopo?**

Kulingana na Ahmad Sheikh Nabhany akinukuliwa katika *Kiswahili Horizons* (Chimerah, 1999) kwamba tunapoṯaka kuḏurusu kuhusu msamiyaṯi au isṯilahi basi tutumiye Suluku ya Ukaribu—kwanza twangaliye lugha za kiSwahili halafu lugha za kiBantu halafu twangaliye lugha nyenginezo sawiya Jeḏwali 1 linatudhihirishiya kwamba mkopano uko kama hali tangavu baina ya lugha za karibu na za mbali. Tuṯaona kwamba japo ‘baba’ na ‘mama’, kwa mfano, ni maneno yanayotumika ulimwengu mzima lakini lugha za kiBantu na za Afrika zaonesha kuwa na maneno yake mbalii kuhusu misamiyaṯi hii miwili na mengineyo. Ise, tata, ishe, pamong’o au nyina, maitũ, inya, nina, koruchon ni nomino zinazowakilisha ‘baba’ na ‘mama’ kimṯawaliya. Na misamiyaṯi mengine ya ukoo ya lugha hizi za kiBantu piya zaṯafauṯiyana na misamiyaṯi ya lugha ‘ngeni’ (za mbali) kiArabu, kiUrḏu, kiIngereza na haṯa kiSanifu kama jeḏwali linavoonesha. Katika kiSanifu, isipokuwa shemeji, shangazi, na mjomba, maneno mengine yoṯʰe yamo katika lugha za kiUrḏu, kiArabu. Hili linatupa sisi ufunuzi kuwa kiSanifu, ambacho nricho ‘kiSwahili’ kilichotangaa mitanraoni na mashuleni, nricho kilichokopa zaiḏi kuṯoka lugha nyengine za mbali kama kiArabu, kiUrḏu kuṯokana na mwingiliyano wake huko kiṯokako: Unguja. Si siri kuwa kiSanifu kilisanifishwa kuṯokana na kiSwahili kizungumzwacho Unguja mjini (Mazrui & Njogu, 2022) na hapo kilikutana na kiUrḏu na/au kiHindi ambapo wazungumzaji wake walikuwa wafanyibiyashara wakubwa Unguja.

**Nomino za mkopo zimo ngeli ipi?**

Kulingana na *Mtalaa wa Isimu* (Mgullu, 1999 uk. 156) ngeli nomino za kimofolojiya katika lugha ya kiSwahili zipo 9 yaani ngeli za: M/MU-WA, M-MI, JI-MA, KI-VI, U-N, U-MA, U-Ø, Ø-MA, ZISIZO NA KIAMBISHI (CHA IDADI) CHOCHOTE (N-N mintarafu ya *Modern Swahili Grammar* [Mohamed, 2001 uk. 43]). Kulingana na Obuchi na Mukhwana (2015 uk. 240) kigezo cha kisemantiki hueleza kuwa JI-MA huhusu: nomino zinazoanza kwa kiyambishi-ngeli ‘ji’ (jani/jino) au ‘Ø’ (paja) katika umoja na ‘ma’ (majani) au ‘me’ (meno) katika wingi; nomino za mkopo katika kiSwahili na yenye kuanza kwa kiyambishi-ngeli ‘ma’ (madaktari) katika wingi bila kujali miyanzo yake ya umoja (daktari). Ngeli ya N nomino zake hazibadiliki katika hali ya umoja na wingi na nyingi ya nomino hizi ni za mkopo kuṯoka lugha nyengine, kwa mfano: simba, kʰuku, samaki, meza, kalamu. Obuchi na Mukhwana (2015 uk. 241) wanaeleza haisṯahiki (sic) kusema shule-mashule, gari-magari.

Mbaabu (1985, uk. 87) anaeleza kuhusu ngeli za baadhi ya ‘majina’ (alivoyaita yeye) ya JI-MA 5/6 yasiyo na kiyambisho cha umoja ni: gari-magari, darasa-madarasa, bonde-mabonde, soko-masoko, duka-maduka. Kwenye ukurasa wa 90 anafafanuwa kwamba baadhi ya majina ya ngeli hizi (N) yaweza pia kuwa na kiyambisho /ma/ katika hali ya wingi. Kwa mfano:

| Ngeli 9 | Ngeli 10 | AU (msisitizo ni wetu) | Ngeli 6 |
|---|---|---|---|
| Gari | gari hizi | | magari haya |
| Darasa | darasa hizi | | madarasa haya |
| Pesa | pesa hizi | | mapesa haya |
| Kamusi | kamusi hizi | | makamusi haya |
| Hospitali | hospitali hizi | | mahospitali haya |

Katika donroo hilo tuṯaona kuwa nomino ambazo asili yake ni za mkopo (ambayo ni mengi sana kulingana na yeye) na piya hazina viyambishi ngeli huwa hivohivo katika umoja na wingi au zaweza kwengezewa /ma/ katika wingi kwa kiSanifu *na isiwe* ni lahaja kwani Obuchi na Mukhwana, na Mbaabu hawakusema hivo. Alhasili, maneno ya mkopo yamo nrani ya kiSwahili na yanapatikana katika ngeli hizi tatu: JI-MA, Ø-MA, N-N. Zawawi (1974) akinukuliwa na Mohamed (2001 uk. 47) anasema kuwa kuna nomino fulani katika kiSwahili ambazo huweza kuwekwa kwenye zaiḏi ya ngeli moja, kwa mfano, 'shangazi wangu', 'shangazi langu', au 'shangazi yangu' zikawa ni ngeli za M-WA, JI-MA, N mtawaliyo. Lakini tufahamu ya kwamba alitumiya 'shangazi' katika umoja ṯu likiwekwa katika wingi sidhani kama kushasikiwa *washangazi wangu uSwahilini.

**Je, wababa au wamama yakubalika?**

Kwa sababu ya kuṯaka kufuwata uwiyano katika ngeli ya M-WA yaani 'wababa' na 'wamama' zikubaliwe zilivo, basi iṯabiḏi tufuwate na masharṯi yake piya: mosi, kwamba iyanze na M (*mbaba, *mmama na jeḏwali letu laonesha hakuna); pili, nomino nyenginezo 'simba', 'ng'ombe', 'mbuzi' 'ḏaktari ('m-nyama' ni umbo lisilo la kawaida [Sacleux, 1939 uk. 578]) piya zikubaliwe kusemwa *wasimba, *wang'ombe, * wambuzi *waḏaktari (ijapokuwa iko Masimba (ni mji Lamu), magombe, mabuzi); na tatu, tugeuze nomino zoṯʰe zilizozoweleka katika kiSwahili: mababu, mabibi, mabwana, manyanya (rejeleya *Utenzi wa Siri li Asrari* wa Mwanalemba (1662)) ziwe *wababu, *wabibi, *wabwana, *wanyanya—na hili ni muhali kufanyika kuṯokana na mmako wa wenye lugha hii (ikiwa wakubaliwa wako).

**Hiṯimisho**

Makala haya yaṉjaribu (kwa ufafanuzi wa /ṉ/ na /me/ rejeleya *Acceptability* (Mazrui, 1981)) kufafanuwa kisarufi maneno 'wababa' na 'wamama' yanayojaribu kujipenyeza katika kiAsiliya (lugha za wenyeji wa mwambawo wa Pwani, Kenya), kwa kuṯojuwa kwa watumiyaji wake kuwa si sahihi haṯa kisarufi. Tumeonesha kuwa 'baba, mama' ni maneno yaso mofimu ya mwanzo Ø, ambayo ni ṯabiya/sifa mojawapo za maneno ya mkopo, na kwamba yaweza kuraṯibishwa katika ngeli kadhaa: wingi wake ukawa ni 'mababa, mamama' ngeli ya JI-MA katika sarufi ya kiSanifu na kiAsiliya na zaweza piya kutumiwa bila 'ma' kwa mfano 'baba zao, mama zao' katika ngeli ya N.

**Nyongeza:** Wakaṯi wa kwelezeya kuhusu ngeli ya U-MA Obuchi na Mukhwana (2015) wanasema kuwa kunayo maneno ya kiBantu ambayo yamo katika ngeli ya 12 na 13 na viyambishi ngeli 'ka' na 'tu' mṯawaliya huwonesha dhana ya udunishaji lakini hayatumiki 'sana' (Iribemwangi, 2008) katika kiSanifu au yanatumika katika maingiliyano 'yasiyo rasmi' (Habwe & Karanja, 2004); na Mbaabu (1985 uk. 83) anaeleza kuwa 'haziko tena' katika kiSwahili. Kulingana na Bakari (1985, kur. 287-8) 'ka' iko katika kiSiu haṯa kiMviṯa imo katika nomino 'Kajimbi', 'Kadingi', kalole (kijito kijidogo), na ḏuka maarufu Marikiti, Mambasa laitwa 'Kwa Katoto'.

**Kongole:** Wa kushukuriwa ni Mola kwa kutuwezesha kwenreleya na juhuḏi zetu katika mwaka mpya wa 2023. Uwe wa ufanisi na maṯarajiyo mema katika masomi yetu. Aidhan, nawashukuru ghaya wanafunzi wangu katika CHAKIKA na Dkt. A. Rotich, ambawo hawawachi kunipa mkono kila nnapowahiṯajiya.

**Kauli Mtakaso:** Baadhi ya nomino katika makala haya zinaweza kuwa ni majina ya watʰu kihalisiya lakini hatukufanya kuwavujiya heshima kwa njiya yoyoṯʰe. Ṯafadhali, naomba, iyeleweke hivo. Tumeyaleta humu kwa sababu ya ṯaalimu ṯu na si zaiḏi ya hilo. Maelezo yaliyomo humu ni yangu na si ya UoK wala Iḏara yetʰu. Kwa loloṯʰe kuhusu makala haya, na Elimu kwa jumla, wasiliyana nami mkarama@kabianga.ac.ke .